# TUJIFUNZE BIBLIA

*SOMO LA 4*

## KULITUMIA KWA HALALI NENO

Katika 2 Timotheo 2:15 twasoma: "***Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu****, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari (yaani, kuona haya),* ***<u>ukitumia kwa halali neno la kweli</u>***." Watu wengi hudhani kwamba watakubaliwa na Mungu mradi wanaisoma Biblia. Walakini mstari huu unatuonya kwamba twaweza kulisoma na kulitumia vibaya neno la Mungu. Tangu siku za Adamu na Hawa hata siku zetu, Shetani amewadanganya watu kwa kulitumia neno la Mungu kwa njia isiyo halali. Tena, **Shetani alijaribu kumdanganya hata Yesu mwenyewe akiyatumia <u>maneno ya Mungu</u> kwa njia isiyo halali** (Mathayo 4:5-7). Basi, katika somo hili twataka kuona jinsi watu wanavyoweza kuitumia vibaya Biblia.

Watu wengi wameshindwa kulitumia kwa halali neno la Mungu wakijaribu kuwalazimisha Wakristo kuzishika sheria ambazo hazituhusu leo. Kwa mfano, baadhi ya watu husema kwamba ni lazima kwa Wakristo kuishika torati.

## JE! TORATI IMEONDOLEWA?

Musa aliviandika vitabu vitano vya Biblia vinavyoitwa **Torati**. Katika vitabu hivi, twasoma habari ya agano ambalo Mungu alilifanya na Waisraeli kwa njia ya mtumishi wake Musa. Katika agano hilo, Mungu aliahidi kuwabariki Waisraeli ikiwa watazishika sheria zake. Watu wengi hudhani kwamba inatakiwa kwa Wakristo kuzishika sheria hizo za torati. Watu hawa wameshindwa kuelewa maneno ya Yesu yafuatayo:

*"Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua torati au manabii; la,* ***sikuja kutangua, <u>bali kutimiliza</u>****. Kwa maana, amin, nawaambia, Mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka,* ***yodi moja wala nukta moja ya torati haitaondoka, <u>hata yote yatimie</u>***." Mathayo 5:17-18

Katika mistari hii, neno <u>hata</u> maana yake ni <u>mpaka</u> kama ilivyo katika <u>Mk 9:1; Mdo 23:12</u>. Basi, Yesu hakusema kwamba torati haitapita <u>kamwe</u>. La! bali alisema **alikuja kuitimiliza torati na kwanba torati haitapita <u>kabla haijatimilizwa</u>**. Biblia inaonyesha waziwazi kwamba torati ilitimilizwa na kuondolewa pia wakati Yesu alipokufa msalabani. Ebu! tuuthibitishe ukweli huu. Baada ya Yesu kufufuka aliwakumbusha wanafunzi maneno yake alkisema:

"*...Hayo ndiyo maneno yangu niliyowaambia nilipokuwa nikali pamoja nanyi, ya kwamba ni <u>lazima yatimizwe yote</u>* ***niliyoandikiwa katika Torati*** *ya Musa, na katika Manabii, na Zaburi...Akawaambia, Ndivyo iliyoandikwa,* ***kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu***." Luka 24:44,46

Tazama! huko juu, Yesu alisema "*yodi moja Wala nukta moja ya torati haitaondoka, hata (au mpaka) yote <u>yatimie</u>*." Kisha, baada ya kufa kwake, Yesu alisema **torati yote <u>ilikwisha kutimilizwa</u> alipokufa na kufufuka!** Kwa hiyo, twasoma:

"Bali **<u>sasa tumefunguliwa katika torati</u>**, tumeifia hali ile iliyotupinga, ili sisi tupate kutumika katika hali mpya ya roho si katika hali ya zamani, ya andiko" Warumi 7:6

Tangu mwanzo haukuwa mpango wa Mungu kwamba Wakristo waishike torati. La! bali torati ilikuwa kiongozi kabla Yesu hajaja. Twasoma:

"*Basi ahadi zilinenwa kwa Ibrahimu na kwa mzao wake. Hasemi, Kwa wazao, kana kwamba ni wengi, bali kana kwamba ni mmoja, Kwa mzao wako, yaani, Kristo…Torati ni nini basi?* ***Iliingizwa kwa sababu ya makosa, hata aje huyo mzao*** *aliyepewa ile ahadi…Lakini* ***kabla ya kuja ile imani tulikuwa tumewekwa chini ya sheria****, tumefungwa mpaka ije ile imani itakayofunuliwa. Hivyo torati imekuwa kiongozi kutuleta kwa Kristo, ili tuhesabiwe haki kwa imani. Lakini,* ***iwapo imani imekuja, hatupo tena chini ya kiongozi***." Wagalatia 3:16,19,23-25

Basi, tusiyatumie vibaya maneno ya Yesu katika Mathayo 5:17-18. Hapo Yesu hakusema kwamba torati itabaki baada ya kutimilizwa. La! bali aliitimiliza torati alipofufuka katika wafu, kisha akaiondoa.

## KWA NINI YESU ALIISHIKA TORATI?

Watu wengi huuliza "kwa nini Yesu aliishika torati ikiwa imeondolewa?" Jibu la swali hili ni kwamba **torati haikuondolewa Yesu alipozaliwa bali iliondolewa alipokufa**. Kwa hiyo, ilimpasa kuishika kabla haijaondolewa. Ebu! tutoe mfano:

Kabla Tanzania haijapata uhuru, tulikuwa chini ya sheria za Wakoloni. Hata Mwalimu Julius K. Nyerere alizaliwa chini ya sheria hizo na kwahiyo, yeye mwenyewe alizishika na kuzifundisha shuleni. Ikiwa angalikuwa mkosefu wa sheria, watu wasingalimtaka kuwa rais wao. Walakini, baada ya Watanzania kupata uhuru, Rais Nyerere hakuzishika tena sheria za Wakoloni. La! Bali aliongoza sheria za wananchi. Vivyo hivyo, Yesu alizaliwa chini ya sheria za Musa. Basi, **Yesu alizishika na kuzifundisha sheria za torati <u>kabla hajafa</u>. Walakini, Yesu alipokufa juu ya msalaba aliondoa sheria zote za Musa akizisimamisha sheria zake mpya**. Ebu! tuthibitishe ukweli huu katika Biblia.

"*Hata ulipowadia utimilifu wa wakati, Mungu alimtuma Mwanawe ambaye amezaliwa na mwanamke,* ***amezaliwa chini ya sheria***." Wagalatia 4:4

Kati ya wanadamu wote ni Yesu tu aliyeweza kuishika torati yote bila kukosa. Kwa hiyo, twasoma:

"*Kwa maana wale wote walio wa matendo ya sheria, wako chini ya laana; maana* ***imeandikwa, Amelaaniwa kila mtu asiyedumu katika yote yaliyoandikwa katika kitabu cha torati, ayafanye****…Kristo alitukomboa katika laana ya torati, kwa kuwa alifanywa laana kwa ajili yetu; maana imeandikwa, Amelaaniwa kila mtu aangikwaye (yaani, kusulibishwa) juu ya mti*." Wagalatia 3:10,13

"*Na kwa sababu hii (Yesu) ni mjumbe wa agano jipya, ili,* ***mauti ikisha kufanyika kwa kukomboa makosa yaliyokuwa chini ya agano la kwanza****, hao walioitwa walipokee ahadi ya urithi wa milele. Maana agano la urithi lilipo, lazima iwepo mauti yake aliyelifanya. Kwa maana* ***agano la urithi lina nguvu palipotukia kufa kwa mtu****; kwa kuwa halina nguvu kabisa, akiwa yu hai yeye aliyelifanya*."
Waebrania 9:15-17

Torati ya Musa iliwatenga watu katika makundi mawili; yaani, Wayahudi na mataifa. Kwa hiyo, torati imeitwa adui yetu. Yesu amewapatanisha Wayahudi na mataifa akiiondoa torati aliposulibiwa. Twasoma:

"*Lakini sasa, katika Kristo Yesu, ninyi mliokuwa mbali hapo kwanza mmekuwa karibu kwa damu yake Kristo. Kwa maana yeye ndiye amani yetu, aliyetufanya sisi sote tuliokuwa wawili kuwa mmoja; akakibomoa kiambaza cha kati kilichotutenga. Naye* ***akiisha kuuondoa <u>ule uadui</u> kwa mwili wake; <u>ndiyo sheria</u>*** *ya amri zilizo katika maagizo; ili afanye hao wawili kuwa mtu mpya mmoja ndani ya nafsi yake; akafanya amani.* ***Akawapatanisha wote wawili*** *na Mungu katika mwili mmoja,* ***kwa njia ya msalaba, akiisha <u>kuufisha ule uadui kwa huo msalaba</u>***." Waefeso 2:13-16

"*Na ninyi (mataifa) mlipokuwa mmekufa kwa sababu ya makosa yenu na kutokutahiriwa kwa mwili wenu, aliwafanya hai pamoja naye, akiisha kutusamehe makosa yote; <u>akiisha kuifuta ile</u>* ***<u>hati</u> iliyoandikwa ya kutushitaki kwa hukumu zake, iliyokuwa na uadui kwetu; akaiondoa <u>isiwepo tena</u>, akaigongomea msalabani; <u>akiisha kuzivua enzi na mamlaka</u>****, na kuzifanya kuwa mkogo kwa ujasiri, akizishangilia* ***<u>katika msalaba huo</u>***." Wakolosai 2:13-16

Kabla Yesu hajafa alifundisha watu kuishika torati. Lakini katika msalaba ndipo alipozivua enzi na mamlaka ya Musa (kama tulivyosoma katika Wakolosai 2:16). Kwa hiyo, baada ya kufufuka kwake twasoma:

"*Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia,* ***Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani***."
Mathayo 28:18

Yesu alisema, "***Yeye anikataaye mimi****, asiyeyakubali maneno yangu, anaye amhukumuye;* ***neno hilo nililolinena ndilo litakalomhukumu siku ya mwisho***." Yohana 12:48

## AGANO LA KALE, AMRI KUMI, NA TORATI YOTE NI MAMOJA

Watu wengi hufikiri kwamba torati ni tofauti na amri kumi na kwamba amri kumi ni tofauti na agano la kale. Kwa sababu wamekosa kuelewa uhusiano uliopo kati ya hayo, ndiyo maana wanashindwa kulitumia kwa halali neno la Mungu. Ukichunguza Biblia, utaweza kuthibitisha kwamba **amri kumi zinaitwa kuwa ni agano la kale** na kwamba **agano la kale linaitwa pia torati**. Ebu! tuone.

Agano maana yake ni mapatano kati ya watu. Katika agano ambalo Mungu alilifanya na Waisraeli, aliahidi kuwapa nchi ya Kanaani na kuwabariki ikiwa watazishika **sheria walizopewa mlimani Sinai**. Kwa hiyo, <u>sheria zile zilikuwa **ndilo agano**</u>. Twasoma:

"*Bwana akasema nanyi kutoka kati ya moto; mkasikia sauti ya maneno, lakaini hamkuona umbo lo lote; sauti tu.* ***<u>Akawahubiri agano lake</u>, alilowaamuru kulitenda, <u>yaani, zile amri kumi;</u>*** *akaziandika juu ya mbao mbili za mawe*" Kumbukumbu 4:12-13

"*Bwana akamwambia Musa, Andika maneno haya; kwa kuwa mimi* ***nimefanya agano nawe, na pamoja na Israeli, kwa mujibu wa maneno haya****... Naye* ***akaandika katika hizo mbao, hayo <u>maneno ya maagano, hizo amri kumi</u>***." Kutoka 34:27-28

Zile mbao mbili za mawe za amri kumi zilitiwa ndani ya sanduku (Kumbukumbu 10:1-5). Basi, **kwa sababu amri kumi zilikuwa ndilo agano, sanduku lile liliitwa "sanduku la agano**." Musa alisema:

"*Naye (Mungu)* ***akaandika juu ya mbao*** *mfano wa maandiko ya kwanza,* ***zile amri kumi****, alizowaambia Bwana huko mlimani toka kati ya moto siku ya mkutano; Bwana akanipa. Basi nikageuka nikashuka kutoka mlimani,* ***nikazitia mbao ndani ya sanduku nililofanya****; nazo zimo humo kama alivyoniamuru Bwana… Na wakati huo Bwana aliitenga kabila ya Lawi ili walichukue* ***lile sanduku la agano la Bwana***." Kumbukumbu 10:4-5,8

Bila shaka tumethibitisha kwamba amri kumi na agano la kale ni mamoja. Basi, sasa twataka kuona kwamba **torati na agano la kale ni mamoja**. Musa aliongoza Waisraeli kutoka Misri mpaka mlima Sinai. Walipofika Sinai, Mungu alianza kuwapa sheria za torati akizitamka zile amri kumi kwa sauti yake mwenyewe. Walakini, kabla Mungu hajamaliza kutoa sheria zote, Waisraeli walimkatisha wakimsihi Musa wakisema: "*Sema nasi wewe, nasi tutasikia, bali Mungu asiseme nasi, tusije tukafa*" (Kutoka 20:29). Basi, Mungu alimwita Musa apande mlimani. Huko mlimani Mungu alimpa Musa zile amri kumi tena pamoja na sheria za torati zilizobaki alipokatishwa. Lakini, kwa sababu **Waisraeli walisikia amri kumi kwa sauti ya Mungu mwenyewe, Mungu aliziandika katika mbao mbili za mawe kuwa ushuhuda juu ya Waisraeli.**

Twasoma, "*Naye akaandika katika hizo mbao, hayo maneno ya maagano hizo amri kumi. Hata ikawa, Musa aliposhuka katika mlima Sinai, na* ***zile mbao mbili za ushuhuda zilikuwa mkononi mwa Musa****, hapo aliposhuka katika mlima, Musa hakujua ya kuwa ngozi ya uso wake iling'aa kwa sababu amesema naye.*" Kutoka 34:28-29

Hata ingawa amri kumi ziliandikwa katika mawe, walakini Mungu alimwamuru Musa kuziandika tena pamoja na sheria zote katika kitabu (chuo) kinachoitwa torati. Twasoma:

"*Basi ikawa hapo Musa alipomaliza kuandika maneno ya torati hii katika chuo, hata yakaisha, ndipo Musa akawaamuru Walawi waliokuwa wakilichukua sanduku la agano la Bwana, akawaambia,* ***Twaeni chuo hiki cha torati, Mkiweke kando ya sanduku la agano la Bwana, Mungu wenu, ili kiwepo kama shahidi juu yako***." Kumbukumbu 31:24-26

Kitabu hiki cha **torati kinaitwa pia kitabu cha agano**. Ndiyo maana **kilitunzwa pamoja na sanduku la agano**. Twasoma: "*Basi Musa akayaandika maneno yote ya Bwana… Kisha akakitwaa kitabu cha agano akakisoma masikioni mwa watu; wakasema, Hayo yote aliyoyanena Bwana tutayatenda, nasi tutatii."*
Kutoka 24:4,7

Twazidi kuthibitisha kwamba amri kumi na torati ni mamoja katika maneno ya mtume. Kwa mfano, twajua kwamba ni amri kumi zilizosema "usitamani". Walakini, mtume alisema "***…singalijua kutamani, kama torati isingalisema, Usitamani.***" Warumi 7:7

### TORATI, AMRI KUMI, NA AGANO LA KALE YOTE YAMEONDOLEWA

Huko juu tulithibitisha kwamba torati, amri kumi, na agano la kale yote ni mamoja. Tena, katika Warumi 7:6-7 na mistari mingineyo, tulisoma kwamba tumefunguliwa katika torati iliyosema "usitamani" (yaani,

amri kumi). Sasa, twataka kuona mistari mingine ya Biblia inayothibitisha kwamba agano la kale limeondolewa. Mungu mwenyewe alitabiri kwamba litaondolewa:

"*Angalia, siku zinakuja, asema Bwana,* ***nitakapofanya agano jipya*** *na nyumba ya Israeli, na nyumba ya Yuda.* ***Si kwa mfano wa agano lile nililolifanya na baba zao, katika siku ile nilipowashika mkono, ili kuwatoa katika nchi ya Misri;*** *ambalo agano langu hilo walilivunja.*" Yeremia 31:31-32

Tunakumbushwa tena maneno hayo hayo ya Mungu katika Waebrania 8:8-12, kisha twasoma: "***Kwa kule kusema, Agano jipya, amelifanya lile la kwanza kuwa kuukuu****. Lakini kitu kianzacho kuwa kikuukuu na kuchakaa* ***ki karibu na kutoweka****.*" Waebrania 8:13

Baada ya Yesu kufufuka twasoma: "*Lakini sasa (Yesu) amepata huduma iliyo bora zaidi, kwa kadiri alivyo* ***mjunbe wa agano lililo bora****, lililoamriwa juu ya ahadi zilizo bora. Maana* ***kama lile la kwanza lingalikuwa halina upungufu, nafasi isingalitafutwa kwa lile la pili.***" Waebrania 8:6-7

"*Na kwa sababu hii (Yesu)* ***ni mjunbe wa agano jipya****, ili, mauti ikiisha kufanyika kwa kukomboa makosa yaliyokuwa chini ya agano la kwanza, hao walioitwa waipokee ahadi ya urithi wa milele… Maana haiwezekani damu ya mafahali na mbuzi kuondoa dhambi. Kwahiyo, ajapo ulimwenguni, asema, Dhabihu na matoleo na sadaka za kuteketezwa na hizo za dhambi hukuzitaka, wala hukupendezwa nazo (zitolewazo* ***kama ilivyoamuru torati****), ndipo aliposema, Tazama, nimekuja niyafanye mapenzi yako.* ***Aondoa la kwanza****,* ***ili kusudi alisimamishe la pili.***" Waebrania 9:15; 10:4-5,8-9

Katika Kutoka 34:27-29, tulisoma jinsi **uso wa Musa ulivyong'aa alipopewa amri kumi** na Mungu. Kwa hiyo, katika mistari ifuatayo, mtume ameziita **amri kumi kuwa ni "hudumu iliyokuja na utukufu."** Basi, tusome kwa makini mistari ifuatayo ili tuone jinsi Biblia inavyofundisha kwamba agano la kale, torati, na amri kumi yote ni mamoja na kwamba yote yameondolewa. Twasoma:

"*Naye (Mungu) ndiye aliyetutosheleza kuwa wahudumu wa* ***agano jipya****; si wa andiko, bali wa roho; kwa maana andiko huua, bali roho huhuisha. Basi ikiwa* ***huduma ya mauti iliyoandikwa na kuchorwa katika mawe*** *(yaani, amri kumi),* ***ilikuja katika utukufu****, hata Waisraeli hawakuweza kuukazia macho uso wa Musa, kwa sababu ya utukufu wa uso wake; nao ni utukufu uliokuwa ukibatilika; je! huduma ya roho haitazidi kuwa katika utukufu?...* ***Kwa maana, ikiwa ile inayobatilika ilikuwa na utukufu, zaidi sana ile ikaayo ina utukufu****. Basi, kwa kuwa tuna taraja la namna hii, twatumia ujasiri mwingi; nasi si kama Musa alivyotia utaji juu ya uso wake, ili kwamba Waisraeli wasitazame sana mwisho wa ile iliyokuwa ikibatilika; ila fikira zao zilitiwa uzito. Kwa maana hata leo hivi, wakati lisomwapo* ***Agano la Kale****, utaji uo huo wakaa; yaani, haikufunuliwa kwamba huondolewa katika Kristo; ila hata leo,* ***torati ya Musa*** *isomwapo, utaji huikalia mioyo yao. Lakini wakati wo wote watakapomgeukia Bwana, ule utaji huondolewa.*" 2Wakorintho 3:6-8,11-16. (Soma pia Wagalatia 4:21-31 na Matendo 15:5-11, 19-29.)

## SHERIA ZA YESU

Mara nyingi, watu wanaposikia kwamba amri kumi za Musa zimeondolewa, baadhi yao husema "Basi, twende tuibe au tuue." Ingawa sheria za Musa zimeondolewa, walakini tupo chini ya sheria za Yesu zilizo kamilifu kuliko sheria za Musa mwenyewe.

"***Amri mpya nawapa, Mpendane***. *Kama vile nilivyowapenda ninyi, nanyi mpendane vivyo hivyo.*"

Yohana 13:34

"*Maana* ***kule kusema, Usizini, Usiue, Usiibe, Usitamani****; na ikiwapo amri nyingine yo yote, inajumlishwa katika neno hili, ya kwamba, Mpende jirani yako kama nafsi yako. Pendo halimfanyii jirani neno baya; basi* ***pendo ndilo utimilifu wa sheria****.*" Warumi 13:9-10

Bila shaka, sheria za Watanzania zimefanana na sheria za zamani za Wakoloni kwa upande na zimepishana kwa upande. Vivyo hivyo, sheria za Yesu na za Musa zimefanana kwa upande na zimepishana kwa upande. Kwasababu zimefanana ndiyo maana watuu wengi wamekosa kupambanua tofauti kati ya sheria za Musa na za Yesu. Walakini, tofauti ni kubwa pia. Ebu, tutoe mifano:

1) Musa aliruhusa watu kutoa talaka na kuoa wake wengi bali Yesu amekataza mambo hayo (soma Mathayo 19:3-9).

2) Musa aliamuru tohara ya kimwili bali Yesu ameamuru tohara ya kiroho (Wagalatia 5:6; 6:15; Wakolosai 2:11; Warumi 2:28-29).

3) Wayahudi walitumia vyombo vya muziki katika kumwimbia Mungu bali Wakristo huimba kwa midomo tu (Wakolosai 3:16).

4) Wayahudi walitoa zaka bali Wakristo hutoa kwa hiara kama walivyofanikiwa (2Wakorintho 9:6-7; 1Wakrointho 16:1-2).

5) Kabla Yesu hajafa, Wayahudi wa zamani waliokolewa bila kubatizwa bali sasa hakuna mtu atakayeokolewa bila kubatizwa (Marko 16:15-16; Matendo 2:38; Yohana 3:3-5; 1Petro 3:20-21; Yakobo 2:24-26).

6) Amri kumi zilihusu matendo yetu bali sheria za Yesu zinahusu matendo na mawazo yetu pia. Yesu alionyesha tofauti kati ya sheria zake na amri kumi za Musa katika Mathayo 5:21-22, 27-28.

7) Amri kumi ziliwaamuru Wayahudi waishike sabato bali Wakristo hushika siku ya kwanza ya juma, yaani Jumapili (Matendo 20:7; 1Wakorintho 16:1-2). Sabato ya Wayahudi imeondolewa; maana Mungu mwenyewe alisema ataikomesha. Twasoma:

"*Tena* ***nitaikomesha*** *furaha yake yote, na sikukuu zake, na siku zake za mwandamo wa mwezi, na sabato zake, na makusanyiko yake yote yaliyoamriwa.*" Hosea 2:11

"*Basi, mtu asiwahukumu ninyi katika vyakula au vinywaji, au kwa sababu* ***ya sikukuu au mwandamo wa mwezi, au sabato****; mambo hayo ni kivuli cha mambo yajayo;* ***bali mwili ni wa Kristo***."

Wakolosai 2:16-17

Sabato maana yake ni kustarehe. Wakristo hutegemea kuingia sabato (starehe) ya Mungu wanapokufa (Waebrania 4:4, 9-11). Basi, sabato ya **Wayahudi iliyoondolewa ilikuwa kivuli au mfano tu wa sabato ya kiroho iliyopo mbinguni.**

**HATUWEZI KUSHIKA SHERIA ZA YESU NA ZA MUSA PIA**

Kabla Yesu hajakufa Mungu aliongoza watu kwa manabii kama Musa bali sasa kiongozi ni Yesu tu.

"***Mungu, ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii*** *kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana, aliyemweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufanya ulimwengu.*" Waebrania 1:1-2

"*Wala **msiitwe** viongozi, maana **kiongozi wenu ni mnoja, naye ndiye Kristo**.*" Mathayo 23:10

Wanafunzi wa Yesu walikosa kuelewa kwamba Musa hana mamlaka. Kwa hiyo, walitaka kuwatukuza Musa na Yesu pia. Ebu, tuone Mungu alivyosema:

"*Na tazama, wakatokewa na Musa na Eliya, wakizungumza naye. Petro akajibu akamwambia Yesu, Bwana, ni vizuri sisi kuwapo hapa; ukitaka, nitafanya hapa vibanda vitatu, kimoja chako wewe, na kimoja cha Musa, na kimoja cha Eliya. Alipokuwa katika kusema, tazama, wingu jeupe likawatia uvuli; na tazama, sauti ikatoka katika lile wingu ikasema, **Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye; msikieni yeye**… Wakainua macho yao, wasione mtu ila Yesu peke yake.*"
Mathayo 17:3-5,8

**Watu wanaotaka kushika sheria za torati leo wako chini ya laana!**

"*Kwa maana wale **wote walio wa matendo ya sheria, wako chini ya laana; maana imeandikwa, Amelaaniwa kila mtu asiyedumu katika yote yaliyoandikwa katika kitabu cha torati, ayafanye**. Ni dhahiri ya kwamba hakuna mtu ahesabiwaye haki mbele za Mungu katika sheria; kwa sababu Mwenye haki ataishi kwa imani… **Mmetengwa na Kristo, ninyi mtakao kuhesabiwa haki kwa sheria; mmeanguka na kutoka katika hali ya neema**.*" Wagalatia 3:10-11; 5:4

**BASI, KWA NINI TUSOME AGANO LA KALE?**

Hata ingawa sisi hatupo chini ya agano la kale siku hizi lakini haina maana kwamba tulitupilie mbali. La! katika Warumi 15:4 twasoma "*kwa kuwa yote yaliyotangulia kuandikwa yaliandikwa ili kutufundisha sisi; ili kwa saburi faraja ya maandiko tupate kuwa na tumaini*" (tazama pia 1Wakorintho 10:11). Kwa hiyo, agano la kale lisomwe kwa uangalifu ili tuone jinsi Mungu alivyowabariki wale waliomtii na jinsi alivyowahukumu wale ambao hawakumtii katika kila kipindi au kizazi. Walakini, tusisahau kwamba sheria za agano la kale zimeondolewa. Ni sheria za Yesu tu zitakazotuokoa au kutuhukumu siku ya mwisho (Yohana 12:48).

**************************************************************************************

Sasa ujibu maswali yanayohusu somo hili, kisha uyapeleke kwa anwani ifuatayo:

***KANISA la KRISTO***

***Tanzania***

## *MASWALI*

1. Je! Mkristo atakayekubaliwa na Mungu ni yule anayetumia neno la kweli kwa njia gani? (2Timotheo 2:15) ____________________
2. Yesu alipokufa na kufufuka aliyatimiliza yote yaliyoandikwa katika nini? (Luka 24:44,46) ___________ na ______________ na ______________
3. Wakristo wamefunguliwa katika nini? (Warumi 7:6) ____________________
4. Torati ilikuwa kiongozi kuwaleta watu kwa nani? (Wagalatia 3:23-25) ____________________
5. Je! Wakristo wapo chimi ya torati (kiongozi) mpaka leo hali imani imekuja? (Wagalatia 3:25) ____________________
6. Yesu alitukomboa katika torati alipoangikwa juu ya nini? (Wagalatia 3:10,13) ____________________
7. Je! agano jipya la Yesu lilikuwa na nguvu kabla Yesu hajafa? (Waebrania 9:15-17) ____________________
8. Katika mauti yake, Yesu aliwapatanisha Wayahudi na mataifa akiziondoa sheria zile za Musa zilizotenga watu akiufisha ule uadui kwa njia ya nini? (Waefeso 2:13-16) ____________________
9. Hati ile iliyoandikwa ya kutushitaki (yaani, sheria za Musa) iliyokuwa na uadui kwetu iliondolewa na kugongomewa wapi? (Wakolosai 2:13-15) ____________________
10. Musa hana mamlaka leo bali mwenye mamlaka yote mbinguni na duniani ni nani? (Mathayo 28:18) ____________________
11. Siku ya mwisho hatutahukumiwa kwa sheria za Musa bali kwa maneno ya nani? (Yohana 12:48) ____________________
12. Je! agano la kale na amri kumi yote ni mamoja? (Kumbukumbu 4:12-13) ____________________
13. Agano la kale (amri kumi) liliandikwa juu ya nini? (Kutoka 34:27-28) ____________________
14. Je! sanduku lile la kuzitunzia zile amri kumi liliitwaje? (Kutoka 34:27-28) ____________________
15. Je! kitabu (chuo) cha torati kiliwekwa kando ya nimi? (Kumbukumbu 31:24-26) ____________________
16. Je! kitabu cha torati kilichoandikwa na Musa kiliitwa pia kitabu cha nini? (Kutoka 24:4,7) ____________________

17. Je! Warumi 7:7 panaonyesha kwamba amri kumi na torati ni mamoja? ____________________

18. Je! Mungu alisema kwamba agano jipya litakuwa sawasawa na agano la kale? (Yeremia 31:31-32) ____________________

19. Kwa sababu agano la kale lilikuwa kuukuu, hata katika siku za nabii Yeremia lilikuwa karibu na kufanya nini? (Waebrania 8:8-12) ____________________

20. Je! agano lililo bora ni agano la kale au agano jipya? (Waebrania 8:6-7) ____________________

21. Yesu alipokuja kufanya mapenzi ya Mungu aliondoa nini ili kusudi alisimamishe agano jipya? (Waebrania 9: 15; 10:4-9) ____________________

22. Katika Kumbukumbu 4:13; 10:4-8; na mistari mingineyo, tulijfunza kwamba amri kumi na agano la kale ni mamoja. Basi, kwa kuwa agano la kale limeondolewa, lazima zile amri kumi nazo zimefanya nini? ____________________

23. Maandiko yanasema amri kumi zilizochorwa katika mawe zilikuwa huduma inayobatilika bali agano jipya ni huduma gani? (2 Wakorintho 3:6-8, 11-16) ____________________

24. Hata leo watu wanaposoma agano la kale (torati, amri kumi) bila kuelewa jinsi Yesu alivyoondoa sheria hizo, utaji huikalia nini? (2 Wakorintho 3:6-8, 11-16) ____________________

25. Amri mpya ya Yesu ni nini? (Yohana 13:34) ____________________

26. Je! ukimpenda jirani yako kama nafsi yako, utaweza kumwua, au kuzini na mke wake, au kutamani mali yake ukaibe? (Warumi 13:9-10) ____________________

27. Upendo ni utimilifu wa ini? (Waruni 13:9-10) ____________________

28. Je! Mkristo akiishika amri ile kuu ya Yesu (upendo) atazihitaji zile amri kumi? (Warumi 13:9-10) ____________________

29. Amri kumi zilizoondolewa ziliamuru watu kushika sabato. Je! mtu ambaye hashiki sabato leo atahukumiwa? (Wakolosai 2:16-17) ____________________

30. Zamani za kale Mungu aliwaongoza baba zetu kwa njia ya manabii kama Musa bali siku hizi amesema na sisi katika nani? (Waebrania 1:1-2) ____________________

31. Kiongozi siye Musa bali ni nani? (Mathayo 23:10) ____________________

32. Je! Mungu anataka tumsikie Musa leo? (Mathayo 17:3-5,8) ____________________

33. Watu wanaotaka kushika sheria za torati leo wako chini ya nini? (Wagalatia 3:10-11; 5:4) ____________________

34. Watu ambao wanataka kushika amri za Musa leo wametengwa na nani? (Wagalatia 5:4) ____________________

*********************************************************************************

Andika jina lako na anwani yako penye nafasi kisha upeleke karatasi hii kwa anwani iliyoandikwa chini ili isahihishwe.

Jina lako …………………………………………………

Anwani yako ……………………………………………

***KANISA la KRISTO***

***Tanzania***